NYAMBARIA HIGH SCHOOL

END OF YEAR EXAMS

Paving Way For Kenya Certificate of Secondary Education Success

Name …….. Admission no…….

Candidate's Signature…… Date…….

FORM 3

KISWAHILI

PAPER 3

TIME: 2Hours

Maagizo

(i) *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

(ii) Jibu maswali ***Matatu*** *pekee.*

(iii) Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

(iv) Fanya Maswali Yote

Kwa matumizi ya mtahini pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
3	20	
JUMLA	60	

SWALI LA KWANZA: USHAIRI. (ALAMA 20)

Wanafunzi sikieni, niwape wangu wasia
Mkiwa mtihanini, muweze kuzingatia
Nataka mtambueni, msije mkajutia
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Kufanikiwa kitaka, watii nao walimu
Sielekeze dhihaka, kwao wao ni muhimu
Kwauliza mwahitajika, maswali yalo magumu
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Mrauke na mapema, msome kwa tumaini
Msije nyie kukwama, kwenye wenu mtihani
Muweze rudia vyema, mlofunzwa awalini
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Umoja ni nguvuni, mwafaa mfahamuni
Jiunge na makundini, masomo mujadilini
Na lile lilo gizani, takuja kulionani
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Ilopita mitihani, Kwa chudi irudieni
Mpate na taswirani, ya ule ulo mwishoni
Ya ziada kazini, ifanye sizembeeni
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Mwelewe sana vyema, yaliyo mtaalani
Msije mkandama, cha mtihani chumbani
Mgongeni ndipo vyema, sije mkapoteani
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Mkiwa madarasani, kelele muepukeni
Sije mkapotezani, muda wenu masomoni
Neneni na vitabu, vitakuja walipani
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Contact 0724333200/0795491185 for marking schemes or order online at
www.kenyaeducators.co.ke

Michezo sipuuzeni, kwayo nyie burudika
Nishati ntapatani, kifurahia michezo
Mazoezi eleweni, ni muhimu kwa ubonge
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Nimefika kaditama, kuweleza ya moyoni
Yafwateni hayo mema, mfaulu mtihani
Ni upuzi msiseme, muda wangu potezeni
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu.

Maswali

a) Eleza mawaidha yanayotolewa Kwa wanafunzi kuhusu namna ya kujitayarisha vyema kwa mtihani. **(alama5)**

b) Eleza umbo la shairi hili. **(alama 4)**

c) Eleza mbinu tatu zilizotumiwa katika shairi hili ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi/ uhuru wa mshairi. **(alama 3)**

d) Taja na utoe mfano wa tamathali moja ya usemi iliyotumiwa katika shairi hili.**(alama1)**

e) Eleza toni ya shairi hili. **(alama 1)**

f) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. **(alama 4)**

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi. **(alama2)**

   i. Dhihaka
   ii. Kaditama

SWALI LA PILI: FASIHI SIMULIZI(ALAMA 20)

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali

Lala mtoto lala*2
Mama atakuja lala
Alienda sokoni lala
Aje na ndizi lala
Na maziwa ya motto lala
Andes lake aciduria
Pia name ya kukupa
Kukupa kwangu wewe kinofu
Kipenzi mwana lala*2

Tija laja*2

Basi kipenzi lala

Baba atakuja lala

Aje na mkate lala

Mkate wa mtoto lala

Tanona ja ndovu lala

Maswali

a) Huku ukithibitisha jibu lako eleza huu ni wimbo wa aina gani? **(alama 2)**

b) Eleza sifa za wimbo wa aina hii. **(alama 5)**

c) Onyesha umuhimu wa wimbo huu. **(alama 4)**

d) Eleza ni shughuli gani za kiuchumi ambazo jamii hii inajihusisha nayo katika wimbo huu. **(alama2)**

e) Tambua mbinu zozote mbili za lugha zilizotumika katika wimbo huu. **(alama 2)**

f) Wimbo huu una wahusika wangapi? Wataje. **(alama 2)**

g) Taja vitendo viwili vinavyoambatana na uimbaji wa aina hii ya wimbo. **(alama 3)**

SWALI LA TATU:TAMTHILIA

***Timothy Arege* : BEMBEA YA MAISHA (ALAMA 20)**

"**Asiyejua safari ya Sara na Yona akielezwa huiona kama f**filamu".

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Bainisha matumizi mawili ya mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo hili. **(alama 2)**

c) Eleza sifa za msemewa. **(alama 4)**

d) Eleza umuhimu wa msemaji. **(alama 5)**

e) Eleza sifa za Yona kama zinavyojitokeza kwenye tamthiliya ya Bembea ya maisha. **(alama 5)**

Contact 0724333200/0795491185 for marking schemes or order online at
www.kenyaeducators.co.ke